**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA DAR ES SALAAM
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz

OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi Kawawa,
S.L.P. 5429,
**12880 – DAR ES SALAAM.**

# TAARIFA KWA UMMA

***Dar es Salaam, 23/09/2025***

Mkoa umepokea kwa masikitiko makubwa picha jongefu kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii ikimuonesha mwalimu akiwaadhibu wanafunzi wa Kidato cha Pili katika Shule ya Sekondari Makumbusho iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kinyume na mwongozo wa utoaji wa adhabu ya viboko. Ufuatiliaji uliofanyika ulibaini kuwa mwalimu aliyehusika ni mwalimu wa **kujitolea** katika shule hiyo. Mkoa unaunga mkono namna Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ulivyochukua hatua za haraka katika kukabiliana na kadhia hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, Toleo la Januari, 2023, wajibu mkuu wa mwalimu ni kuhakikisha anachukua hatua zinazofaa kuhakikisha mwanafunzi analindwa dhidi ya aina zote za ukatili kama vile ubaguzi, unyanyasaji na uchapaji viboko usiozingatia taratibu. Kitendo chochote cha adhabu ambacho kitasababisha madhara ya kimwili kwa mwanafunzi hakiruhusiwi. Hata hivyo, kwa kubaini kuwa wapo wanafunzi ambao wawapo shuleni huonesha utovu wa nidhamu na kusababisha walimu kuchukua hatua ikiwemo kuwaadhibu; Serikali kupitia Wizara ya Elimu ilitoa Waraka wa Elimu Na. 24 wa Mwaka 2002 kuhusu Adhabu ya Viboko ambapo waraka huo umefafanua kikamilifu hatua za kumwadhibu mwanafunzi aliyefanya makosa ndani au nje ya shule.

Kufuatia tukio hilo, Uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni umechukua hatua zifuatazo:-

I. Kwanza, Mkoa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni umesikitishwa sana na tukio hilo ambalo pamoja na kusambaa kwake, pia limeleta taharuki na sura isiyofaa kwa Wananchi kwa ujumla;

II. Ufuatiliaji umefanyika kuhusu wanafunzi walioadhibiwa na kwamba afya zao ni njema na wanaendelea na masomo yao kama kawaida;

III. Mkoa na Halmashauri tunaendelea kushirikiana na Uthibiti Ubora wa Shule ambao wanaendelea kuchunguza ili kuhakikisha haki na usalama wa wanafunzi unasimamiwa vizuri;

IV. Kufuatia tukio hilo, maelekezo yametolewa kwa Wakuu wa Shule wote kuhakikisha wanatoa maelekezo fasaha kwa walimu wote wanaojitolea katika shule zao kuhakikisha wanazingatia Taratibu, Kanuni na Sheria pamoja na kuzingatia waraka Na 24 wa mwaka 2002 wa utoaji wa adhabu katika shule zao; na

V. Kufanya ufuatiliaji wa kina kuhusu tabia na mienendo ya walimu wanaoomba ajira ya muda katika shule husika kabla ya kuwaajiri (Kutumia Mwongozo wa Walimu wa Kujitolea katika Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Tanzania Bara, Toleo la Juni, 2023).

.........................

Adrophina M. Ndyeikiza

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**OFISI YA MKUU WA MKOA**
**DAR ES SALAAM**